

COUNTY GOVERNMENT OF LAMU



THE COUNTY ASSEMBLY OF LAMU

THE HANSARD

Wednesday, 8th July, 2026

*The Assembly met at the
Main Chambers, at 10:30 a.m.*

[Temporary Speaker (MCA Beatrice Wamaitha Munge) in the Chair]

PRAYERS

Temporary Speaker (MCA Beatrice Wamaitha Munge): Next Order.

Clerk-at-the-Table: Motion.

MOTION

*Improvement of main access roads through installation of culverts, proper drainage systems
and street lighting in Lamu County*

Temporary Speaker (MCA Beatrice Wamaitha Munge): Honorable Members, aware that the mover of this motion is not in the House at the moment, we therefore defer this motion to the next session today in the afternoon.

Next Motion.

Outbreak of dengue fever and chikungunya in Lamu County

MCA Aisha Ali Abdulrahman (*Nominated*): Thank you Madam Temporary Speaker. Madam Temporary Speaker, I beg to move the following motion: -

AWARE THAT, Article 43(1)(a) of the Constitution of Kenya, 2010 guarantees every person the right to the highest attainable standard of health, including the right to healthcare services.

FURTHER AWARE THAT, County governments are responsible for County health services under part 2 of the Fourth Schedule to the Constitution.

CONCERNED THAT, Lamu County has recently experienced an outbreak of dengue fever and chikungunya, which are mosquito-borne viral diseases that pose a significant threat to public health, livelihoods, education, tourism and economic activities within the County.

NOTING THAT, the diseases are characterized by high fever, severe headaches, joint and muscle pains, fatigue, skin rashes and in severe cases may lead to hospitalization and other serious health complications.

FURTHER NOTING THAT, the spread of the diseases has been exacerbated by poor waste management, stagnant water, inadequate public awareness and insufficient vector control measures in some parts of the County.

COGNIZANT THAT, timely intervention through surveillance, vector control, public sensitization, provision of medical supplies and intergovernmental collaboration is critical in containing the outbreak and safeguarding public health.

NOW THEREFORE, this County Assembly resolves that the County Executive Committee Member responsible for health: -

1. Declares the dengue fever and chikungunya outbreak a matter of urgent public health concern and submits to the County Assembly within fourteen

- (14) days, a comprehensive status report on the extent of the outbreak, affected areas, responsible measures undertaken and challenges encountered.
2. Intensifies disease surveillance, testing, diagnosis, treatment and reporting mechanisms in all health facilities across the County.
 3. Undertakes immediate countywide mosquito control interventions including fumigation, elimination of mosquito breeding sites, drainage of stagnant water, environmental sanitation campaigns and proper waste management.
 4. Launches an aggressive public awareness and health education campaign through radio stations, social media platforms, public meetings, schools, religious institutions and other appropriate channels to educate residents on prevention and control measures.
 5. Ensures adequate availability of medicines, testing kits, protective equipment and healthcare personnel in all public health facilities to effectively manage affected patients.
 6. Collaborates with the Ministry of Health, Kenya Medical Research Institute (KEMRI), development partners and other relevant agencies to mobilize technical and financial support for outbreak containment.
 7. Establishes a County Emergency Response Team to coordinate interventions and provide weekly updates on the status of the outbreak until it is fully contained.
 8. Submits quarterly reports to the County Assembly on the implementation of the interventions and the progress made in controlling the outbreak.

Madam Temporary Speaker, may I elaborate further. Recently in our County we are experiencing a lot of problems like joint pains and fevers which end up causes chikungunya according to laboratory staffs. For our people to be helped, let the County Government take action by employing health workers who will survey every wards and come up with a better solution.

Second

MCA Hope Wanjiku Mwaura (Nominated): Asante sana Bi Spika. Bi Spika nimesimama kuchangia na pia kuunga mkono hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Aisha Abdulrahman. Bi Spika kiukweli katika Kaunti hii yetu ya Lamu kila Wadi idadi nyingi ya wananchi wanaugua maradhi ya chikungunya na dengue fever. Bi Spika mada hii imetueleza ya kwamba ni haki ya kila mkenya kupata matibabu yanayofaa. Kwa hivyo hoja hii ni muhimu sana na ni hoja inayowahusu wananchi wa Kaunti hii yetu ya Lamu. Pia idara hiyo hiyo ya afya inafaa kuwahamasisha umma namna ya kujikinga na maradhi haya. Nakumbuka katika Wadi yetu ya Bahari tuliweza kumzika Mzee ambaye alikuwa akifanya kazi katika benki ya equity aliuguwa ugonjwa wa dengue fever na baada ya muda akafariki. Kwa hivyo ningemalizia kwa kuwanasihia Waheshimiwa wenzangu waweze kuchangia hoja hii ili tuweze kulitatua tatizo hili sugu.

Motion Proposed**Members Contributions**

MCA Barisa Deko Bana (Basuba): Asante sana Bi Spika kwa kunipa nafasi ya kuunga mkono hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Aisha Abdulrahman. Bi Spika katika Wadi yangu ya Basuba tuliweza kumpoteza kijana wa miaka mitano ambaye alikuwa akiuguwa ugonjwa wa chikungunya. Kwa hivyo ningeiomba Idara ya afya ichukuwe hatua muafaka ya kuweza kulitatua donda hili sugu. Nakumbuka kitambo idara ya afya ilikuwa ikikaguwa kila nyumba na kutafuta suluhu mbadala ya kutatua maradhi haya lakini siku hizi naona wamezembea sana licha ya ugatuzi kuanzishwa nchini.

Na la kusikitisha Zaidi ni kwamba ni miaka 13 sasa tangu Serikali za ugatuzi zianzishwe na mpaka sasa hakuna mikakati yoyote imepangwa katika Idara hii ya afya. Na kama wameona mapato yao ni kidogo ya kuwawezesha kuwafikia wananchi katika kila wadi basi watuandikie barua sisi wanakamati wa kamati ya

bajeti nikiwa Mwenyekiti wa kamati hiyo tutaweza kuwaruhusu watumie pesa za dharura ili waweze kulitatua tatizo hili sugu haswahaswa msimu huu wa mvua.

MCA James Njaaga Kariuki (Hindi): Asante sana Bi Spika kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Bi Spika, kwanza ningependa kumpongeza Mheshimiwa Aisha Abdulrahman kwa kuuleta mswada huu hapa Bungeni. Tutakubaliana kwa pamoja kwamba saa hii kila familia katika Kaunti hii yetu ya Lamu inakumbana na ugonjwa wa dengue fever. Na ni masikitiko makubwa sana kuona tuko na Wizara ya afya na ugonjwa huu unazidi kuenea na bado hawautilii maanani mpaka tumefikia mahali tunaujadili hapa Bungeni.

Na tukiangalia kumetolewa tahadhari ya mvua kali na watabiri wa hali ya hewa, maji yataweza kukaa kwenye vidimbwi na mbu wataanza kuzaana kwenye vidimbwi hivyo. Ndiposa nikasema ni wakati mwafaka wa Wizara husika kuchukua hatua zifaazo na hata sisi Waheshimiwa tunafaa kufuatilia kwa karibu na kuhakikisha Wizara ya afya imeweka mikakati gani ya kupigana na janga hili kwa sababu wananchi wanaumia sana. Tukiangalia pesa ziko kwa sababu Mwenyekiti wa kamati ya bajeti amesema wametenga pesa za kutosha za kupigana na majanga kama haya. Kwa hivyo namalizia kwa kuunga mkono mswada huu.

MCA Mercy Riziki Nzai (Nominated): Asante sana Bi Spika kwa kunipa fursa ya kuchangia mswada ulioletwa na Mheshimiwa Aisha Abdulrahman. Bi Spika kama tujuavyo huu ni msimu wa mvua na maji yamesimama kila mahali na kusababisha mbu kuzaana kila uchao. Kama Waheshimiwa wenzangu walivyosema huu ni wakati mzuri kwa Waziri wa afya kuingia nyanjani na kuwaeleza wananchi kuhusu janga hili na namna ya kujikinga na janga hili. Kwa hivyo namalizia kwa kuunga.

MCA Mercy Wangeci Nyambura (Nominated): Thank you Madam Speaker, I rise to support the motion. Madam Speaker, we all know that prevention is better than cure. With the support brought by my fellow Members we urge our residents to look at their surroundings by clearing the bushes, draining stagnant water in their areas in order to prevent the spread of dengue fever. And also in the sensitization the

County Government should also teach the residents about the symptoms of dengue fever.

MCA Somoe Abdulrahman Mahmoud (*Nominated*): Asante Bi Spika kwa kunipa fursa ya kusimama na kuunga mkono mswada ulioletwa na Mheshimiwa Aisha Abdulrahman. Kama tujuavyo wananchi wanasikitika sana haswahaswa pale gati la Mokowe maji yakisimama msimu huu wa mvua basi mbu huzaana kwa wingi. Kwa upande wa shuleni yale matanki ya maji hayatiwi madawa ya kuuwa vidudu vinavyozaana ndani ya maji hayo na pindi wanafunzi wanapokunywa maji hayo basi hupata maradhi na hatimaye kufariki wakiwa wadogo.

Mover's Response

MCA Aisha Ali Abdulrahman (*Nominated*): Asante sana Bi Spika, pili ningependa kuwashukuru Waheshimiwa waliochangia mswada niliyoulela hapa Bungeni.

(Question put and agreed upon)

ADJOURNMENT

Temporary Speaker (MCA Beatrice Wamaitha Munge): Honorable Members, there being no other business, the Assembly stands adjourned until today Wednesday 8th July 2026 at 2:30pm

The Assembly rose at 11:30am